HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA.

OFISI YA AFISA MTENDAJI WA KATA,
KATA YA TEMBELA,
S.L.P. 149,
MBEYA.
09/05/2007.

Kumb. Na. AF/KT/TEMB/VOL.II/41/07.

THE FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY,
HAIDERY PLAZA, GHOROFA YA 5, MTAA WA UPANGA/KISUTU,
S.L.P. 7192,
DAR ES SALAAM.
TANZANIA.

YAH: UDF KUINGIA KATIKA KINYANG'ANYIRO CHA ASASI BORA.

Somo la hapo juu lahusika.

Katika Mafunzo yaliyofanywa na UDF Katika eneo letu yaliyofanyika Mwezi March 2007, Baada ya Mafunzo hayo, Mambo yafuatayo yaliibuka Katika kata yetu:

1. Tumepanga kufyatua tofali 24,000 Kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ya Kata.
2. Kumeibuka tatizo la wizi mdogo mdogo wa kuibiana Mazao Kama vile Mahindi wakati wa kukomaa, Kata imeunda kamati za Mitaa za Ulinzi na Usalama ili kudhibiti suala zima la wizi huo.

**NB**: Kutoka kwenye Kata yetu mpaka zahanati ilipo ni Km 20, wazazi hujifungua njiani.

Sisi Kama Kata tumefurahishwa sana na Mafunzo hayo ya Kuwaelimisha wananchi juu ya kujua haki zetu. UDF wamekuwa wawazi sana Katika Kutuelimisha.

Tunaomba au kushauri waingizwe Kwenye Kinyang'anyiro hicho Cha Asasi bora za Tanzania.

Ndimi Katika Kazi.

Thadeo Daniel Deo.
AFISA MTENDAJI WA KATA.
TEMBELA.

AFISA MTENDAJI
KATA YA TEMBELA